

Kategoria za Maneno zenye Sinonimu za Asili na za Mkopo katika Kiswahili

*George J. Kitundu*¹

Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam

*Pendo S. Malangwa*²

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ikisiri

Ukopaji wa maneno katika lugha ni mbinu mojawapo ya lugha kujitajirisha kimsamiati. Kuwapo kwa maneno ya mkopo katika lugha husababisha lugha kopaji kuwa na msamiati changamani, yaani msamiati wa asili na wa mkopo. Lugha inapokuwa na msamiati changamani hutokea wakati neno la asili linakuwa na kisawe kutoka lugha ngeni moja au zaidi, hivyo, kuibua sinonimu za asili na za mkopo, yaani neno moja ni la asili na lingine/mengine ni ya mkopo. Baadhi ya wataalamu kama vile Sarma, Bharali, Mahanta, Sakia na Sarmah (h.t); Kreidler (1998), Gelderen (2002), Griffith (2006) pamoja na Khamisi (2014) wanaeleza kuwa sinonimu katika lugha hujidhihirisha katika kategoria mbalimbali za maneno. Wataalamu hao wanaendelea kudai kuwa kati ya kategoria hizo zipo zenye sinonimu nyingi na nyingine zina sinonimu chache. Lugha ya Kiswahili inadhihirisha sifa ya kuwa na maneno ya asili na ya mkopo kutokana na kukopa maneno mengi kutoka lugha za kigeni (Chuwa, 1988; Besha, 1995; Kiango, 1995; King'ei, 2010; Matinde, 2012). Kuwapo kwa maneno ya mkopo kunasababisha lugha hii kuwa na msamiati changamani, na hivyo, kuwa na sinonimu zenye asili tofauti. Sinonimu hizo, kama ilivyoelezwa, zinajitokeza katika aina mbalimbali za maneno. Licha ya kujitokeza katika kategoria mbalimbali za maneno, bado suala hili halijawa wazi sana katika lugha ya Kiswahili hususani kategoria zenye sinonimu pamoja na kiwango cha ujitokezaji wa sinonimu katika kategoria hizo. Kwa hiyo, makala haya yanahusu kategoria za maneno zenye sinonimu za asili na za mkopo. Data za makala haya zimekusanywa kutoka matini za kamusi ambazo ni *Kamusi ya Visawe* (KV) (2014), *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (KKK) (2017) na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (KKS) (2019). Data zilizokusanywa zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data kimaudhui na kiulinganishi. Ufafanuzi na ufasiri wa data zilizotumika umeongozwa na misingi ya Nadharia ya Vijenzi Maana.

1.0 Utangulizi

Katika lugha kuna maneno ambayo yanahusiana kimaana. Maneno hayo hujulikana kama sinonimu. Hali ya maneno kuwa na maana sawa au zilizokaribiana inaitwa usinonimu ilhali maneno yenye sifa hiyo huitwa sinonimu (taz. Ullmann, 1967; Harris, 1973; Ndimele, 1997; Kahigi, 2019; TUKI, 2019;

¹ **Baruapepe:** *george.jerald@yahoo.com*

² **Baruapepe:** *pmalangwa@yahoo.co.uk*

Chacha na Malangwa, 2019). Sinonimu katika lugha zinaweza kuwa za asili tu, yaani zisizohusisha neno la mkopo, za mkopo tu ambazo hazihusishi neno la asili au zenye asili tofauti, yaani zile zinazohusisha neno moja la asili na lingine la mkopo. Makala haya yanachunguza sinonimu zenye asili tofauti. Sinonimu zenye asili tofauti katika lugha hutokana na sababu kubwa ya ukopaji wa maneno kutoka lugha mbalimbali za kigeni (Kiango, 1999; King'ei, 2010; Khamis, 2014; Resani, 2015; Chacha na Malangwa, 2019). Lugha inapokuwa na maneno ya mkopo na ya asili husababisha lugha kopaji kuwa na msamiati changamani, yaani msamiati wa asili na wa mkopo (Kiango, 1999). Msamiati wa asili ni ule ambao hautokani na ukopaji wa maneno kutoka lugha za kigeni. Msamiati huu katika kamusi nyingi za Kiswahili kama KKK (2017) na KKS (2019) hubainika kwa kukosa taarifa ya kietimolojia, jambo linaloashiria kuwa msamiati huo ni wa asili ya Kiswahili. Msamiati wa kigeni ni ule ambao unatokana na ukopaji wa maneno kutoka lugha za kigeni. Msamiati huu katika KKK (2017) na KKS (2019) umebainishwa kwa kuwekewa taarifa ya kietimolojia. Kuwapo kwa msamiati wa asili na wa mkopo katika lugha hutokea wakati neno la asili likawa na kisawe kimoja au zaidi kutoka lugha ngeni moja au zaidi. Hali hiyo huibua sinonimu ambazo huhusisha neno la asili na lingine la mkopo kutoka lugha ngeni moja au zaidi. Maelezo ya wataalamu wengi kama Sarma, Bharali, Mahanta, Sakia na Sarmah (h.t), Gelderen (2002), Kreidler (1998), Griffith (2006) na Khamisi (2014) yanaonesha kuwa sinonimu katika lugha zinajitokeza katika kategoria mbalimbali za maneno. Kati ya aina hizo, kuna baadhi yake zinaonekana kuwa na kiwango kikubwa cha sinonimu kuliko kategoria nyingine huku kategoria zingine zikionekana kutokuwa na sinonimu kwa kuwa hazitajwi katika maandiko ya wataalamu mbalimbali. Mifano ya kategoria zenye sinonimu ni nomino (N), kitenzi (T), kielezi (E), kivumishi (V) na kihusishi (H). Kwa upande mwingine, mifano ya kategoria ambazo zinaonekana kutokuwa na sinonimu katika maandiko ya wataalamu mbalimbali ni kihisishi (H), kiunganishi (U) na kiwakilishi (W). Ingawa maelezo ya wataalamu hao yanahitimisha hivyo, lakini hitimisho hilo si majumui kwa lugha zote kwa sababu lugha zinatofautiana kitabia. Hivyo, upo uwezekano wa kuwa na mfanano na/au utofauti katika vipengele mbalimbali. Kwa hiyo, jambo hili la kategoria za maneno zenye sinonimu linapaswa kuchunguzwa katika lugha mahususi. Kwa mantiki hiyo, makala haya yamechunguza kategoria za maneno zenye sinonimu katika lugha ya Kiswahili. Katika uchunguzi huo, kwanza tumefafanua dhana ya sinonimu na aina zake kisha tumefafanua dhana ya kategoria za maneno pamoja na aina za maneno zenye sinonimu. Pili, tumejadili kiunzi cha kinadharia kilichoongoza makala haya sambamba na kubainisha mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu. Baada ya ufafanuzi wa vipengele hivyo, uchambuzi na ufafanuzi wa data umefanyika. Mwisho wa makala haya tumetoa hitimisho la makala nzima.

2.0 Sinonimu kwa Ujumla

Sinonimu ni maneno yenye maana zinazokaribiana au zilizo sawa (Grey, 1964; Harris, 1973; Palmer, 1976; Robins, 1980; Lyons, 1995; Ndimele, 1997; Saeed, 1997; Cruce, 2000; Cruce, 2006; Griffiths, 2006; Hurford, Heasley na Smith, 2007; Matei, 2008; Massamba, 2009; Matinde, 2012; Skallman, 2012; Habwe na

Karanja, 2015 na Resani, 2015 na TUKI, 2019). Maneno huwa sinonimu katika lugha moja pale sifa za kisemantiki katika maneno hayo zinapofanana, yaani sifa hizo zinajitokeza katika pande zote mbili za maneno yanayojenga seti ya sinonimu (Kreidler, 1998; Cruse, 2006 na Riemer, 2010). Mathalani, neno *hard* (ugumu) lina sifa ya kuwa *tough* (ugumu/uzito) (na neno *difficult* (ugumu/ngumu) pia lina sifa hiyo ya kuwa *tough* (ugumu). Kwa hiyo, maneno *hard/difficult* ni sinonimu kwa sababu yote yana sifa ya *tough* inayojitokeza katika maneno hayo (Kreidler, 1998). Kreidler (1998) anadai kuwa kadiri sifa zinavyolingana ndivyo kiwango cha usinonimu kati ya maneno hayo kinavyozidi kuongezeka. Kwa hiyo, kiwango cha usinonimu katika maneno hutegemea zaidi sifa za kisemantiki zinazohusiana. Hivyo, ni dhahiri kuwa baadhi ya jozi za sinonimu zitakuwa na kiwango kikubwa cha usinonimu kuliko jozi zingine (Ndimele, 1997; Kreidler, 1998). Maelezo haya yana maana kuwa usinonimu una viwango fulani katika lugha. Kuwapo kwa viwango hivyo kunatupatia aina mbili za sinonimu, yaani sinonimu kamili na zisizo kamili.

Sinonimu kamili ni zile ambazo zinaweza kutumika katika miktadha tofautitofauti bila kuathiri maana (Palmer, 1976; Chacha na Malangwa, 2019; Kahigi, 2019). Sinonimu hizi zinapotumika katika miktadha mbalimbali huwa na maana na athari ileile. Mathalani, *semasioloji/sarufi-maana/semantiki, sauti ya nazali/sauti ya king'ong'o, sarufi maumbo/mofolojia na sarufi-miundo/sintaksia* (Ullmann, 1967; Resani, 2015; na Kahigi, 2019). Sinonimu zisizo kamili ni zile ambazo zinaweza kubadilishana matumizi katika baadhi tu ya miktadha. Sinonimu hizi huweza kuwa na athari sawa katika baadhi ya miktadha lakini zikatofautiana katika miktadha mingine (Dixon, 1991; Ndimele, 1997; Riemer, 2010). Riemer (2010) anafafanua zaidi hoja hii kwa kutumia mfano wa maneno *pupil* (mwanafunzi) na *student* (mwanafunzi). Anadai kuwa maneno haya yanakuwa sinonimu tu kama yatahusisha muktadha wa shule au elimu kwa maana ya mtu anayefundishwa na mwalimu. Ikiwa *pupil* itarejelea jicho basi maneno hayo si sinonimu. Hivyo, *pupil* na *student* ni moja ya mifano ya sinonimu zisizo kamili kwa sababu zinahusiana katika moja ya dhana zake tu. Mfano mwingine wa sinonimu zisizo kamili ni *saumu* na *kwaresma* ambazo zinarejelea dhana ya kujinyima chakula kwa lengo la kutafuta fadhila za kidini. Ingawa dhana inayorejelewa na maneno hayo ni moja lakini yanatofautiana katika muktadha wa matumizi ambapo *saumu* hutumiwa na Waislamu na *kwaresma* hutumiwa na Wakristo. Kipengele kinachofuata kinafafanua chanzo cha sinonimu za asili na za mkopo.

2.1 Chanzo cha Sinonimu

Sinonimu huibuka kutokana na sababu mbalimbali. Hata hivyo, kwa minajili ya makala haya tutajadili chanzo cha sinonimu hususani za asili na za mkopo. Sababu kubwa ya kuwapo kwa maneno ya mkopo katika lugha ambayo ndiyo yanasababisha kuibuka kwa sinonimu zenye asili tofauti ni ukopaji. Kwa hiyo, kipengele hiki kinajadili ukopaji wa maneno katika lugha na namna unavyoibua sinonimu zenye asili tofauti.

Moja ya sababu kubwa za kuwapo kwa sinonimu hususani za asili na za mkopo katika lugha, ni ukopaji wa msamiati kutoka lugha mbalimbali za kigeni. Kiango (1999) na King'ei (2010) wanaeleza kuwa ukopaji wa maneno si suala la lugha fulani maalumu tu, bali ni mbinu ya kukuza lugha inayotumiwa na lugha zote duniani. Ukopaji wa maneno uko wa namna mbili. Kwanza, ni kukopa kutoka lugha ambazo kiisimu ziko katika familia moja. Mathalani, lugha ya Kiswahili hukopa maneno kutoka lugha zingine za Kibantu ambazo zina mnasaba na Kiswahili. Pili, ni kukopa kutoka lugha za kigeni ambazo zinatofautiana kiisimu (Kiango, 1999).

Lugha ya Kiswahili, kama zilivyo lugha zingine nayo imekopa maneno kutoka lugha mbalimbali za kigeni (Chuwa, 1988; Basha, 1995; Kiango, 1999; Chacha na Malangwa, 2019). Maneno katika lugha hayakopwi tu kiholela bali kuna sababu mbalimbali zinazochoea. Kwanza, ukopaji wa neno hutokana na mahitaji ya msamiati katika lugha kwa ajili ya kuelezea dhana fulani. Gray (1964), Kiango (1999) na Matinde (2012) wanaeleza kuwa ukopaji wa neno hufanyika ikiwa neno linalokopwa linasimamia dhana ngeni au kitu ambacho hakikuwa kinajulikana katika jamii ya lugha hiyo. Kutokana na ukopaji huu, msamiati wa kigeni huelezea dhana husika ambapo dhana hiyo haina kisawe chake katika lugha ya asili. Kwa hiyo, ukopaji wa namna hii huwa hauongezi visawe kwa sababu maneno hukopwa ili kuelezea dhana ambazo hazijulikani katika lugha husika. Pili, ukopaji wa msamiati kutokana na kasumba ya wazungumzaji wa lugha fulani kupenda kukopa msamiati kutoka lugha mbalimbali ingawa msamiati unaorejelea dhana hiyo upo katika lugha yao. Kiango (1999) na Matinde (2012) wanaeleza kuwa wazungumzaji wa lugha wana kasumba ya kukopa msamiati kutoka lugha mbalimbali za kigeni hata kama msamiati unaosimamia dhana hiyo upo katika lugha yao. Kwa hiyo, istilahi inaweza kukopwa si kwa sababu haipo katika lugha inayohusika, bali ni kwa sababu istilahi inayokopwa inatoka katika lugha bora zaidi ya lugha yao. Hali hii husababisha msamiati wa lugha chanzi kuonekana kuwa bora zaidi kuliko msamiati wa asili ulio kwenye lugha kopaji (Matinde, 2012). Mathalani, maneno kama *kompyuta*, *televisheni* na *stendi* huonekana bora zaidi kuliko visawe vyake vya asili kama *tarakilishi*, *runinga* na *kituo cha mabasi*. Tatu, kuwapo kwa maingiliano ya nguvu kisiasa na kiuchumi pia husababisha jamii kutumia maneno ya lugha tawala, na hivyo, kuongeza msamiati katika lugha tawaliwa ingawa msamiati unaoelezea dhana hiyo ulikuwepo katika lugha yao (Robins, 1964; Chuwa, 1988). Kiango (1999) anatoa mfano wa Wagiriki kuwa kutokana na kuwa na ushawishi mkubwa katika nyanja za sayansi, sanaa na falsafa, walifanya msamiati wao ukopwe sana katika lugha ya Kilatini. Hali hii pia imewahi kujitokeza katika lugha ya Kiswahili ambapo kulikuwa na mwingiliano na jamii zenye nguvu za kisiasa, hasa wakati wa ukoloni wa Waingereza na Wajerumani. Katika kipindi hicho maneno mengi yalitoholewa kutoka lugha za Kiingereza na Kijerumani kuja lugha ya Kiswahili (Kiango, 1999). Hii ndiyo maana kuna jozi mbalimbali za sinonimu kama *shule/skuli*.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, ni dhahiri kuwa ukopaji unaotokana na kasumba ya watu kukopa msamiati kutoka lugha za kigeni iwe kwa kutawaliwa au kwa nia ya

kujifarahisha, ndiko kunakosababisha kuibuka kwa sinonimu zenye asili tofauti. Hii ni kwa sababu katika maingiliano ya lugha moja na nyingine, watu hukopa msamiati toka kwenye lugha hizo ilhali msamiati unaodokeza dhana hizo upo katika lugha yao jambo ambalo huibua sinonimu. Inapotokea kukawa na mwingiliano wa jamii kopaji na jamii nyingine tena, wazungumzaji wazawa hukopa tena msamiati unaoelezea dhana ileile hata kama walikwishakopa kutoka lugha zingine. Jambo hili husababisha kuwe na maneno matatu au manne kutoka lugha nne tofauti zenye kuelezea dhana ileile, yaani sinonimu.

Kiswahili ni moja ya lugha zenye maneno ya mkopo kutoka lugha mbalimbali za kigeni. Kwa hiyo, lugha hii ina msamiati changamani, yaani msamiati wa asili na wa mkopo. Chuwa (1988) aliwahi kusema kuwa Kiswahili kinajengwa na msamiati changamani ambapo kati ya msamiati huo asilimia 72.17 inahusisha maneno kutoka lugha za asili (yaani lugha za Kibantu), asilimia 22.92 kutoka lugha ya Kiarabu, asilimia 2.09 kutoka lugha ya Kiingereza, asilimia 1.04 kutoka Kireno, asilimia 1.72 kutoka Kihindi na asilimia 0.06 kutoka lugha zingine kama Kituruki na Kifaransa. Kuwapo kwa msamiati changamani kama tulivyodokeza awali, husababisha lugha kuwa na sinonimu za asili na za mkopo kwa sababu visawe vingi vya mkopo huongezewa juu ya maneno ya asili, na hivyo, kuibua sinonimu (Chacha na Malangwa, 2019). Ukopaji wa maneno unahusisha kategoria mbalimbali za maneno (McMahon, 1994; Kreidler, 1998). Ufafanuzi wa kategoria za maneno zenye sinonimu unatolewa katika kipengele kinachofuata.

2.2 Kategoria za Maneno zenye Sinonimu

Kategoria ni jumla ya vitu vya aina fulani vinavyoweza kuwekwa pamoja kwa mujibu wa sifa zinazofanana (Matinde, 2012; TUKI, 2019). TUKI (2019) wanaendelea kueleza kuwa maneno huwekwa katika makundi mbalimbali yenye sifa zinazofanana kisarufi kama vile nomino, kitenzi au kivumishi. Kundi la maneno yenye sifa zinazofanana huitwa kategoria za kileksika au kategoria za maneno. Maneno katika kategoria au kundi moja huweza kuwa na kisawe chake cha kategoria hiyohiyo kutoka lugha zingine hali ambayo inaibua sinonimu zinazohusisha kategoria fulani. Kipengele hiki kinafafanua kategoria za maneno zenye sinonimu zenye asili tofauti.

Sinonimu kama ambavyo tumefafanua awali, ni maneno yenye maana zinazofanana au kukaribiana. Kwa kuwa ni maneno na kuna kategoria mbalimbali za maneno, ni dhahiri kuwa sinonimu zinajitokeza katika aina mbalimbali za maneno. Haya yanaelezwa pia na Sarma, Bharali, Mahanta, Sakia na Sarmah (h.t) kuwa sinonimu katika lugha zinajitokeza katika aina mbalimbali za maneno. Wanaendelea kueleza kuwa ingawa katika lugha ya Assamese kuna sinonimu nyingi zinazohusisha kategoria za nomino, kitenzi, kielezi na kivumishi lakini kuna kila dalili kwamba kategoria za kisarufi kama kihusishi, kiunganishi na kihisishi huenda nazo zina sinonimu. Maelezo hayo yanadhihirisha kuwa sinonimu zinajitokeza katika aina mbalimbali za maneno ingawa zaidi ni kwa kategoria za nomino, kitenzi, kielezi na kivumishi. Kategoria zingine hususani za kisarufi inaelekea kuwa hazina sinonimu ingawa hakuna uhakika wa kuwapo kwake.

Kwa upande wake McMahon (1994), anaeleza kuwa ukopaji wa maneno unahusisha aina mbalimbali za maneno ingawa zaidi unahusu maneno yenye ujazo kamili kama vile vitenzi na nomino. Anaendelea kueleza kuwa kati ya kategoria hizo, nomino ndiyo kategoria inayokopwa zaidi kuliko kategoria zingine huku vitenzi vikifuatia na baadaye vivumishi. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa maneno mengi yanayokopwa yanahusisha kategoria ya nomino, kitenzi na kivumishi. Kulingana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa kategoria hizo ndizo zenye sinonimu nyingi za asili na za mkopo kwa kuwa visawe vingi vya kigeni (vya kategoria hizo) huongezewa juu ya maneno ya asili (ya kategoria hizo). Baadhi ya kategoria kama kielezi, kihisishi, kiwakilishi, kiunganishi na kihusishi ambazo hazikubainishwa na McMahon kama zinakopwa pia, na hivyo, huenda hazina sinonimu au zina kiasi kidogo tu.

Nao Kreidler (1998) na Gelderen (2002) wanaeleza kuwa sinonimu katika lugha zinajitokeza katika aina mbalimbali za maneno kama vile nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi na kihusishi. Kreidler (1998) anafafanua zaidi kwa kutoa baadhi ya mifano kama vile *hide/conceal* (kitenzi), *skinny/thin/slender* (kivumishi) na *postman/mailman* (nomino), inayodhihirisha kuwapo kwa kategoria za maneno zenye sinonimu. Ingawa wataalamu hao haweki wazi, ni dhahiri kuwa aina hizo ndizo zenye sinonimu kuliko aina zingine ambazo hazajibainisha kama kiunganishi, kiwakilishi na kihisishi.

Griffith (2006) naye anaeleza kuwa kategoria mbalimbali za maneno zina sinonimu. Kategoria hizo ni pamoja na kivumishi, kielezi, nomino, kihusishi na kitenzi. Griffith anatoa mifano ifuatayo kushadadia hoja yake: (*Truck-lorry*) (nomino); (*Depart-leave*) (kitenzi); (*Quickly-fast*) (kielezi); (*Outside-without*) (kihusishi); na *Rich-wealthy* (kivumishi). Maelezo ya Griffith yanadhihirisha kuwa kategoria za nomino, kitenzi, kielezi, kihusishi na kivumishi ndizo zenye sinonimu ilhali kategoria ambazo hazajibainisha kama kihisishi, kiwakilishi na kiunganishi hazina sinonimu. Pamoja na kwamba Griffith amebainisha kategoria za maneno zenye sinonimu lakini haweki wazi suala la kiwango cha sinonimu katika kategoria hizo, yaani zipi zina sinonimu nyingi kuliko zingine, jambo ambalo limeshughuliwa katika makala haya.

Khamisi (2014) naye anaeleza kuwa sinonimu zinajitokeza katika aina mbalimbali za maneno ingawa hujidhihirisha zaidi katika nomino kuliko kategoria zingine. Maelezo ya mtaalamu huyu yanaashiria kuwa sinonimu zinajitokeza zaidi katika kategoria mbalimbali ingawa zaidi ni kwa nomino. Hivyo, kwa maelezo yake inaelekea kuwa kategoria zote zina sinonimu lakini zaidi ni kwa nomino, jambo ambalo kwa hakika si tu kwamba linatia shaka bali linahitaji uchunguzi zaidi. Kwa ujumla, maelezo ya wataalamu wengi yanaonesha kuwa sinonimu zinajitokeza katika aina mbalimbali za maneno. Kati ya aina hizo, kuna baadhi ya kategoria kama nomino inaonekana kuwa zina kiwango kikubwa cha sinonimu kuliko kategoria zingine. Aidha, maelezo yao yanaonesha kuwa baadhi ya kategoria kama kiwakilishi na kiunganishi hazina sinonimu katika lugha. Ingawa

maelezo ya wataalamu hao yametusadia kufahamu kategoria za maneno zenye sinonimu na zisizo na sinonimu lakini maelezo yao hayatoshi kuhitimisha suala hili kwa sababu lugha zinatofautiana kitabia ndio maana kati ya waliojadiliwa wapo wanaosema ziko tano na wengine wakitaja pungufu ya tano huku wengine wakitaja kategoria ya kihusishi ilhali wengine hawaitaji. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa jambo hili linapaswa kuchunguzwa kimahususi. Makala haya yanafafanua kategoria za maneno zenye sinonimu hususani za asili na za mkopo kwa kutumia mifano kutoka lugha ya Kiswahili. Kipengele kinachofuata kinajadili kiunzi cha kinadharia.

2.4 Kiunzi cha Kinadharia

Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Vijenzi Maana. Nadharia hii iliibuka mwishoni mwa miaka ya 1950 na mwanzoni mwa miaka ya 1960 huko Ulaya na Marekani. Ingawa nadharia hii iliibuka kutokana na mawazo ya wanamuundo wa kifonolojia ambao waliitumia katika kutofautisha fonimu katika lugha, lakini kwa Ulaya iliibuka kutoka katika Nadharia ya Kikoa Leksika wakati Marekani ilichipuka kutoka kwa wanaisimu anthropolojia kama vile Kroeber, Conklin na Lounsbury. Kwa upande wa Ulaya, mawazo ya nadharia hii yanajitokeza katika kazi za Eugenio Coseriu, Bernard Pottier na Algirdas Greimas katika miaka ya 1960 (Geeraerts, 2009). Kahigi (2019) anaeleza kuwa uchanganuzi wa namna hii una chimbuko katika mkabala wa lugha ulioenezwa na kitabu cha de Sassure (1916) na waanzilishi wa uchanganuzi wa kimuundo wa msamiati wa lugha walikuwa Trier (1934) na Porzig (1934) ambao walikuwa wa kwanza kuchambua vikoa maana. Kahigi (2019) anaendelea kudai kuwa toka kipindi hicho wanasemantiki wengi wamechanganua msamiati kwa kutumia mkabala wa vikoa maana na, pia, vijenzi semantiki wakiwamo Nida (1975) na Lyons (1977).

Nadharia hii inaegemea katika msingi kuwa maneno yanajengwa na vijenzi fulani ambavyo vinaweza kubainishwa, na hivyo, kuelezea neno hilo. Vijenzi hivyo vinabainishwa na Weisgerber kuwa ni jenda au koo (Geeraerts, 2009; Kahigi, 2019). Vijenzi vya kila neno ndivyo vinavyojenga maana ya jumla ya kila neno na vijenzi hivyo ndivyo hutofautisha au kuonesha uhusiano uliopo baina ya maneno yaliyo katika kikoa kimoja. Kwa hiyo, leksimu zote zaweza kuchanganuliwa kwa kutumia seti siukomo ya vijenzi-semantiki ambavyo ni vya kijumla (Geeraerts, 2009; Kahigi, 2019). Mathalani, leksimu *mwanamke* maana yake huweza kubainishwa kwa vijenzi au nduni tatu: *mtu*, *mtu mzima* na *me* (Kahigi, 2019). Kijenzi semantiki *mtu* humtofautisha na viumbe ambavyo sio watu. Kijenzi *mtu mzima* humtofautisha mwanamke na msichana au mwanaume na mvulana na kijenzi *me* humtofautisha mwanamke na mwanamume. Kwa kifupi nduni hizo huonekana kama ifuatavyo: *Mwanamke* = [+MTU], [+MTU MZIMA], [-ME]. Katika nadharia hii, alama [+] huashiria kuwapo kwa kijenzi husika ilhali alama [-] huashiria kutokuwapo kwa kijenzi husika. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu nadharia hii tutazame mfano wa kikoa cha maana cha samani katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Kikoa cha Maana cha Samani

Kikoa cha Samani	Kiegemeo cha Nyuma	Yenye Miguu	-A Kukalia	Enye Vishikio
<i>Kiti</i>	+	+	+	-
<i>Sofa</i>	+	+	+	+
<i>Kigoda</i>	-	+	+	-

Chanzo: Kahigi (2019)

Katika Jedwali Na. 1 tunaona kikoa cha samani cha *kiti*, *sofa* na *kigoda*. Katika kikoa hicho, vijenzi maana vinaonesha kuwa kiti cha kawaida hakina mshikio huku kigoda kikiwa hakina kiegemeo cha nyuma (Kahigi, 2019). Kwa hiyo, kutoka katika mfano huo maana ya kiti ni kifaa kilichotengenezwa kwa ajili ya kukalia na ambacho kina egemeo kwa nyuma, miguu na vishikizo. Mfano huu wa kikoa pia unadhihirisha kuwa maneno yanayojenga kikoa maana cha samani kama *kiti*, *sofa* na *kigoda* yana sifa ya usinonimu kwa sababu yanafanana katika baadhi ya vijenzi vyake hususani dhana ya kuwa na miguu na -a kukalia (sehemu ya kukalia). Kwa hiyo, nadharia hii imetumika kubaini maneno yenye kufanana kimaana kwa kuangalia mfanano wa vijenzi maana vyake. Maneno yenye vijenzi maana vilivyo sawa au vinavyokaribiana ni sinonimu. Aidha, nadharia hii haiishii tu kubainisha maneno yenye sifa ya usinonimu bali kuonesha kiwango cha usinonimu katika maneno hayo. Ikiwa maneno yanafanana katika vijenzi maana vyote ni dhahiri kuwa maneno hayo yana kiwango kikubwa cha usawe lakini ikiwa yanafanana katika baadhi tu ya vijenzi maana vyake ni dhahiri kuwa maneno hayo yana kiwango kidogo cha usawe. Kipengele kinachofuata kinafafanua mbinu mbalimbali za utafiti.

3.0 Mbinu za Utafiti

Data za utafiti huu zimekusanywa kutoka matini tatu za kamusi. Kamusi hizo ni *Kamusi ya Visawe* (2014), *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2017) na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2019). Sampuli ya matini hizo imetokana na mbinu ya usampulishaji kwa madhumuni maalumu. Matini za KKS na KKK zimeteuliwa kwa sababu ndizo kamusi pekee zinazoandaliwa na Taasisi³ kongwe za uandaaji wa kamusi za TATAKI (KKS) na BAKITA (KKK). Pia, kamusi hizo zina taarifa za sinonimu pamoja na etimolojia ya vidahizo vyake, data ambazo ndio msingi wa utafiti huu. Kwa upande wa kamusi ya KV nayo imeteuliwa kwa sababu ndiyo kamusi pekee katika lugha ya Kiswahili inayohusika visawe tu, data ambayo ndiyo msingi wa kufikia mahitimisho ya utafiti huu. Data kutoka matini hizo zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data kimaudhui na kiulinganishi (Ragin, 1987; Kombo na Tromp, 2006). Kutoka katika matini hizo jumla ya seti 65 za sinonimu za asili na za mkopo zilikusanywa. Kipengele kinachofuata kinawasilisha na kuchambua data zilizokusanywa.

³ *Kamusi ya Kiswahili Fasaha* (KKF) kutoka BAKIZA haikuhusishwa kwa sababu haihusishi taarifa ya etimolojia ambayo ndiyo msingi wa kufikia mahitimisho ya makala haya.

4.0 Katgoria za Maneno zenye Sinonimu za Asili na za Mkopo

Kipengele hiki kinawasilisha na kuchambua data zilizokusanywa kutoka matini teule. Kulingana na uchambuzi wa data imebainika kuwa sinonimu za asili na ya mkopo katika Kiswahili zinajitokeza katika katgoria mbalimbali za maneno. Katgoria zilizobainika ni pamoja na nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi, kihisishi na kiunganishi. Ufafanuzi wa katgoria hizo unatolewa katika vipengele vinavyofuata.

4.2.1 Sinonimu za Katgoria ya Nomino

Nomino ni maneno yanayotaja majina ya watu, vitu, hali, viumbe, dhana au matendo (Kihore, 2009; Khamisi, 2009). Nomino ni moja ya katgoria za maneno zenye sinonimu za asili na za mkopo. Hii inajidhihirisha kupitia data zilizokusanywa ambapo kati ya seti 65 za sinonimu, kuna seti 30, sawa na asilimia 46, zinazohusisha katgoria ya nomino. Katika seti hizo, neno moja ni la asili la Kiswahili huku mengine yakiwa ni ya mkopo kutoka lugha mbalimbali za kigeni ambazo zilikuwa na muwasala na lugha ya Kiswahili. Seti za sinonimu zinazohusisha katgoria ya nomino zinawasilishwa kwa muhtasari katika majedwali Na. 2 na Na. 3:

Jedwali Na. 2: Sinonimu za Katgoria ya Nomino

Na.	Asili ya Neno					Fahiwa Jumuishi (Kijenzi/vijenzi maana Jumuishi)	
	Kiswahili	Kiarabu	Kiingereza	Kiajemi	Kireno	Kihindi	
1.	Mhuni			Jambazi			Mtu mwenye tabia ya kihuni enye kuiba kwa kutumia silaha
2.	Utingo		Taniboi				Mwenye kupandisha na kushusha mizigo katika gari msaidizi wa dereva
3.	Mkurufunzi		Kocha				Mwalimu wa michezo
4.	Mtunzafedha	Mhasibu					mtu anayetunza fedha na hesbu
5.	Mpatanishi	Msuluhishi	Modereta				Mtu anayesuluhisha watu waliogombana
6.	Mfuafedha					Sonara	Mtu mtengeneza vitu kutokana na madini ya fedha
7.	Muuguzi		Nesi				Mtu anayefanya kazi ya kuhudumia wagonjwa muuguzi wa wagonjwa hospitalini
8.	Mwamuzi		Refa				Mwamuzi wa mchezo kama vile mpira
9.	Mkayakaya		Mkrismasi				Mti wenye umbo la mwavuli, vijani vidogo, maua ya rangi nyekundu au manjano na tumba bapa ndefu
10.	Mkandarasi		Kontrakta				Mtu anayefanya ujenzi kwa mkataba maalumu
11.	Mkorosho				Mbibo	Mkanju	Mti mwenye kuzaa mabibo
12.	Kimatu			Maige			Mtoto wa nzige ambaye hajaanza kupuruka

Na.	Asili ya Neno					Fahiwa Jumuishi (Kijenzi/vijenzi maana Jumuishi)	
	Kiswahili	Kiarabu	Kiingereza	Kiajemi	Kireno	Kihindi	
13.	Katibu muktasi	Mhazili		Karani			Mtu anayetunza barua na majalada ya ofisi pamoja na kuandika au kutaipu
14.	Mpakizi	Hamali	Kuli				Mtu anayefanya kazi ya kupakia na kupakua mizigo bandarini au forodhani
15.	Mtarijumani	Mkalimani	Mtapta				Mtu afasiriaye papo kwa papo mazungumzo kutoka lugha moja kwenda nyingine

Chanzo: Data za Maktabani (2020)

Data za Jedwali Na. 2 zinahusisha sinonimu za kategoria ya nomino. Seti hizo zinahusisha maneno ya asili ya Kiswahili na ya mkopo kutoka Kiarabu, Kiingereza, Kiajemi, Kireno na Kihindi. Data katika Jedwali hilo zinaonesha kuwa maneno mengi yanayohusisha kategoria ya nomino yametoholewa kutoka lugha ya Kiingereza kuliko lugha zingine. Maneno hayo ni pamoja na *taniboi*, *kocha*, *modereta*, *nesi*, *refa*, *mkrismasi*, *kontrakta*, *kuli* na *mtapta*. Lugha zingine kama Kiarabu, Kituruki, Kihindi, Kiajemi na Kireno nazo zina maneno ya mkopo yanayohusisha kategoria ya nomino ingawa kwa uchache hasa unapozilinganisha na lugha ya Kiingereza. Mathalani, lugha ya Kiarabu ina maneno kama *mhasibu*, *msuluhishi*, *mhazili*, *hamali* na *mkalimani* huku kukiwa na maneno *jambazi*, *maige* na *karani* kutoka Kiajemi; *mkanju* na *sonara* kutoka Kihindi; na *mbibo* kutoka Kireno. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa kutokana na utohozi wa maneno kutoka lugha za kigeni kuna sinonimu zenye asili tofauti ambazo zinahusisha kategoria ya nomino. Ili kuendelea kupata uangavu zaidi kuhusu sinonimu zinazohusisha kategoria ya nomino tutazame data zingine katika Jedwali Na. 3.

Jedwali Na. 3: Sinonimu za Kategoria ya Nomino

Na.	Asili ya Neno				Fahiwa Jumuishi (Kijenzi/vijenzi maana Jumuishi)
	Kiswahili	Kiarabu	Kiingereza	Kihindi	
1.	Mwandani	Rafiki			Mtu anayependwa sana na watu.
2.	Garimoshi		Treni		Gari linaloenda juu ya reli lenye mabehewa mengi
3.	Kibago		Stuli		Kimeza kidogo kinachotumika kuwekea vitu au miguu
4.	Karakara		Pesheni		tunda lenye mbegu nyeusi na hutumiwa kuetngenezewa juisi
5.	Ganja	Kasumba		Bangi	Kileo kinachotokana na mimea kama bangi
6.	Ambo	Sherishi	Gluu	Gundi	Kitu kama gundi kinachonata
7.	Kichapuzi		Aksereta		Kifaa maalumu katika chombo cha moto cha kuongeza kasi
8.	Fimbo	Bakora			Fimbo ya kutembelea pigo la fimbo
9.	Shombe	Suriama	Hafukasti	Chotara	Mtu aliyezaliwa na wazazi wa rangi mbalimbali

Na.	Asili ya Neno				Fahiwa Jumuishi (Kijenzi/vijenzi maana Jumuishi)
	Kiswahili	Kiarabu	Kiingereza	Kihindi	
10.	Mganga	Tabibu	Daktari		Mtu anayefanya kazi ya kutibu wagonjwa
11.	Bikizee	Ajuza			Mwanamke mzee sana
12.	Nyanya			Bibi	Mama mzaa baba au mama
13.	Zeruzeru		Albino		Mtu ambaye ngozi yake na nywele vinakosa rangi ya asili
14.	Mwanamaji	Baharia			Mfanyakazi wa chombo cha baharini
15.	Kijasumu		Bakteria		Viumbe wadogo sana wasioonekana kwa macho wenye kusababisha maradhi

Chanzo: Data za Maktabani (2020)

Jedwali Na. 3 linaonesha kwa muhtasari data zaidi zinazohusisha kategoria ya nomino. Kama ilivyokuwa kwa Jedwali Na. 2, Jedwali hili pia tunaona sehemu kubwa ya maneno yamekopwa kutoka lugha ya Kiingereza na Kiarabu, na hivyo, kuwa na sinonimu nyingi zinazohusisha kategoria ya nomino kutoka lugha hizo. Mathalani, maneno ya mkopo kutoka lugha ya Kiingereza ni pamoja na *treni*, *stuli*, *pesheni*, *gluu*, *akseleleta*, *hafukasti*, *daktari*, *albino* na *bakteria*. Maneno kutoka Kiarabu ni pamoja na *rafiki*, *kasumba*, *sherishi*, *bakora*, *suriama*, *tabibu*, *ajuza* na *baharia*. Lugha ya Kihindi nayo ina maneno yanayohusisha kategoria ya nomino katika Kiswahili. Maneno hayo ni pamoja na *bangi*, *gundi*, *chotara* na *bibi*. Kwa hiyo, kutokana na Kiswahili kutohoa maneno kutoka lugha mbalimbali za kigeni kuna sinonimu zinazohusisha kategoria ya nomino kwa sababu maneno mengi ya mkopo ya kategoria ya nomino yanafanana kimaana na maneno ya asili ya kategoria ya nomino. Kipengele kinachofuata kinawasilisha data zinazohusisha kategoria ya kitenzi.

4.2 Sinonimu za Kategoria ya Kitenzi

Vitenzi ni maneno yanayoelezea tendo linalofanywa na nomino (Kihore, 2009; Khamisi, 2009). Kitenzi ni moja ya kategoria za maneno zenye sinonimu zenye asili tofauti. Hii inajidhihirisha kupitia data zilizokusanywa ambapo kati ya seti 65 za sinonimu, kuna seti 25, sawa na asilimia 38 zinazohusisha kategoria ya kitenzi. Hivyo, ni dhahiri kuwa sinonimu zinazohusisha kategoria ya kitenzi nazo zinajitokeza kwa wingi ingawa si kama ilivyo kwa nomino. Data za kategoria hii zinawasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 4.

Jedwali Na. 4: Sinonimu za Kategoria ya Kitenzi

Na.	Asili ya Neno					Fahiwa Jumuishi (Kijenzi/vijenzi maana Jumuishi)
	Kiswahili	Kiarabu	Kiingereza	Kiajemi	Kihindi	
1.	Kopesa				Pepesa	Peleka kope juu na chini
2.	Hesabu/jumlisha	Adidi				Tafuta hesabu ya watu au vitu
3.	Faa	Afiki				Kubali fikra au hoja fulani
4.	Agiza	Amuru				Ambia mtu afanye jambo fulani.
5.	Agua	Tabiri				Eleza au toa habari ya mambo yatakayotokea
6.	Kemea	Laumu				Toa mtu makosa
7.	Maliza	Kamilisha				Bila ya kuzidi au bila kupungua
8.	Komesha/zuia	Akifisha				Zuia jambo lisifanyike
9.	Alika	Karibisha				Ita watu kwenye sherehe
10.	Amkia	Sabahi				Taka mtu hali
11.	Andaa	Adidi			Tayarisha	Weka tayari
12.	Shindwa		Feli			Shindwa katika mtihani
13.	Julisha	Arifu	Ripoti			Julisha mtu habari ya jambo fulani
14.	Haini	Asi				Kataa kutii amri
15.	Chachisha		Asidisha			Fanya kitu kipate chachu
16.	Kisia	Kadiria		Bahatisha		Jaribu kupata jambo bila ya kujua matokeo yake
17.	Donea		Kisi	Busu		Piga kisi
18.	Pasua			Chana		Paua kitu kama nguo au karatasi
19.	Egesha		Paki			Weka pembeni chombo cha usafiri kama vile jahazi, gari au baiskeli
20.	Kagua		Cheki			Tazama kwa madhumuni ya kusahihisha
21.	Taarifu/eleza	Habarisha	Ripoti			Toa maelezo juu ya mtu, kitu au jambo fulani
22.	Vamia	Hujumu				Shambulia bila ya kuwa na haki ya kufanya hivyo
23.	Pima	Ratili				Tafuta kiasi kama vile urefu au upama wa kitu
24.	Pungua	Adimika				Patikana kwa uchache
25.	Chelewa	Ahiri				Kuwa nyuma ya wakati mahususi uliowekwa

Chanzo: Data za Maktabani (2020)

Jedwali Na. 4 linaonesha sinonimu za asili na za mkopo zinazohusisha kategoria ya vitenzi. Seti hizo zinahusisha maneno ya asili ya Kiswahili na yale ya Kiswahili yenye asili ya kigeni kutoka lugha ya Kiarabu, Kiingereza, Kiajemi na Kihindi. Katika data hiyo maneno mengi yanayohusisha kategoria ya vitenzi yametoholewa kutoka lugha ya Kiarabu huku yakifuatiwa na lugha ya Kiingereza. Hii ni kwa sababu katika data hiyo kuna vitenzi 18 vya Kiswahili vyenye asili ya Kiarabu. Vitenzi hivyo ni pamoja na *adidi, afiki, tabiri, laumu, kamilisha, akifisha, sabahi, adidi, amuru, karibisha, arifu, asi, kadiria, habarisha, hujumu, ratili, adimika* na *ahiri*. Vitenzi vyenye asili ya Kiingereza vilivyotoholewa ni pamoja na *ripoti, cheki, paki, kisi, asidisha, ripoti* na *feli*. Lugha ya Kiajemi inafuatia ya Kiingereza kwa sababu ina vitenzi 3 ambavyo ni *bahatisha, busu* na *chana* huku Kihindi kikiwa na maneno mawili ya kategoria ya kitenzi ambayo ni *tayarisha* na *pepesa*. Data hiyo inaonesha kuwa kuna utohoaji mkubwa wa maneno yanayohusisha vitenzi kutoka Kiarabu kuliko lugha zingine kama Kiingereza, Kiajemi na Kihindi. Kwa hiyo, katika lugha ya Kiswahili kuna sinonimu zinazohusisha kategoria ya kitenzi. Kategoria nyingine ya kielezi inafafanuliwa katika kipengele kinachofuata.

4.3 Sinonimu za Kategoria ya Kielezi

Kielezi ni neno linalotoa habari juu ya tendo katika sentensi. Vielezi hueleza tendo linafanywa wakati gani, linafanywa wapi, linafanywa mara ngapi na linafanywa namna gani (Kihore, 2009; Khamisi, 2009). Kategoria hii ina sinonimu za asili na za mkopo kutoka lugha mbalimbali za kigeni. Kati ya data zilizokusanywa imebainika kuwa kategoria ya kielezi ina seti 4 za sinonimu, sawa na asilimia 6. Idadi hii inaonesha kuwa kuna ujitokezaji mdogo wa sinonimu zinazohusisha kategoria ya kielezi kuliko kategoria za nomino na kitenzi. Data za kategoria ya kielezi zinawasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 5.

Jedwali Na. 5: Sinonimu za Kategoria ya Kielezi

Namba	Asili ya Neno				Fahiwa Jumuishi (Kijenzi/vijenzi maana Jumuishi)
	Kiswahili	Kiarabu	Kiajemi	Kihindi	
1.	Vizuri	Sawasawa	Barabara		Kama inavyotakiwa
2.	Ange			Tayari	Kwa hali iliyokamilika
3.	Polepole	Taratibu		Asteaste	Kwa taratibu
4.	Tele	Mzo		Chakari	Zaidi ya kawaida kupindukia/mpaka juu

Chanzo: Data za Maktabani (2020)

Jedwali Na. 5 linaonesha seti za sinonimu zinazohusisha kategoria ya kielezi. Seti hizo zinahusisha maneno ya asili ya Kiswahili na yale ya Kiswahili yenye asili ya mkopo kutoka lugha ya Kiarabu kama maneno *sawasawa, taratibu* na *mzo*; kutoka Kiajemi kama *barabara* na Kihindi chenye maneno *tayari, asteaste* na *chakari*. Data hiyo inaonesha wazi kuwa maneno mengi yanayohusisha kategoria ya kielezi yanakopwa kutoka lugha za Kiarabu na Kihindi huku kukiwa na ukopaji mdogo kutoka lugha ya Kiajemi. Baadhi ya lugha kama Kiingereza, Kituruki na Kifaransa kulingana na data yetu hazina maneno yanayohusu kategoria ya kielezi katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, katika lugha ya Kiswahili kutokana na lugha hii

kutohoa maneno ya mkopo yanayohusisha kategoria ya kielezi, kuna sinonimu zinazohusisha kategoria hiyo ambapo neno la asili linafanana kimaana na neno la mkopo. Ufafanuzi wa kategoria nyingine ya maneno yenye sinonimu unatolewa katika kipengele kinachofuata.

4.4 Sinonimu za Kategoria ya Kihisishi

Vihisishi ni maneno yanayodokeza hisia za msemaji kama vile furaha, kushangaa, kuumia au kuudhika (Kihore, 2009). Aina hii ya maneno pia huitwa viingizi. Jina la kihisishi linatokana na dhima yake ya kutokea hisia mbalimbali kama furaha au huzuni. Kategoria hii ina sifa mbili; kwanza inahusisha sauti inayotumika katika kutamka maneno hayo na pili ni kuwa na kawaida ya kutangulizwa katika tungo (Kihore, 2009). Sifa ya kwanza ndiyo inayofanya aina hii ya maneno kuitwa vihisishi kwa kuwa huonesha hisia mbalimbali za msemaji. Sifa ya pili ndiyo inayofanya aina hii ya maneno iitwe viingizi, yaani kitangulizi cha tungo. Hii ina maana kuwa viingizi mara nyingi hutangulia tungo. Katika lugha ya Kiswahili kuna sinonimu zinazohusisha kategoria ya kihisishi. Hii inajidhihirisha kupitia data zilizokusanywa ambapo kati ya seti 65 za sinonimu, kuna seti 3 za sinonimu, sawa na asilimia 5 zinazohusisha kategoria ya kihisishi. Data hizo zinaoneshwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 6.

Jedwali Na. 6 : Sinonimu za Kategoria ya Kihisishi

Na.	Asili ya Neno						Fahiwa Jumuishi (Kijenzi/vijenzi maana Jumuishi)
	Kiswahili	Kiarabu	Kiingereza	Kiajemi	Kireno	Kihindi	
1.	Kamwe!	Abadani!				Bilikuli!	Hata kidogo!
2.	Abaa!		Aisee!				Neno la kumfanya mtu asikilize habari unayotaka kumuambia
3.	Angalia!	Simile!		Habedari!	Heria!		Tamko la kutahadharisha kuhusu jambo fulani kuwa makini

Chanzo: Data za Maktabani (2020)

Jedwali Na. 6 linaonesha seti 3 za sinonimu zinazohusisha kategoria ya kihisishi. Seti hizo zinahusisha maneno ya asili ya Kiswahili na maneno ya Kiswahili yenye asili ya kigeni kutoka Kiarabu, Kihindi, Kiingereza, Kiajemi na Kireno. Maneno mengi yanayohusisha kategoria hii yametoholewa kutoka Kiarabu kuliko lugha zingine. Maneno yenye asili ya Kiarabu yaliyotoholewa ni pamoja na *abadani!* na *simile!* Huku baadhi ya lugha zikiwa na neno mojawoja kama Kiingereza (*aisee!*), Kiajemi (*habedari!*), Kireno (*heria!*) na Kihindi (*bilikuli!*). Kwa hiyo, katika lugha ya Kiswahili, kutokana na lugha hii kutohoa maneno kutoka lugha mbalimbali za kigeni, kuna vihisishi vilivyotoholewa kutoka lugha hizo, na hivyo, kutengeneza seti kadhaa za sinonimu za asili na za mkopo ingawa ni kwa uchache sana inapolinganishwa na kategoria za nomino, kitenzi na kielezi. Kategoria ya kivumishi inafafanuliwa katika kipengele kinachofuata.

4.5 Sinonimu za Kategoria ya Kivumishi

Neno kivumishi hutokana na neno kuvumisha, yaani kutoa habari au kueneza habari. Kwa hiyo, vivumishi ni maneno yanayokumusha nomino ama kueleza habari ya mtu jinsi alivyo au kitu jinsi kilivyo, kinavyoonekana au jinsi kinavyofikiriwa kwamba kina tabia fulani au kipo katika idadi fulani (Kihore, 2009; Khamisi, 2009). Katika lugha ya Kiswahili kuna sinonimu zenye asili tofauti zinazohusisha kategoria ya kivumishi. Hii inajidhihirisha kupitia data zilizokusanywa ambapo kati ya seti 65 za sinonimu, kuna seti 2 za sinonimu, sawa na asilimia 3 zinazohusisha kategoria ya kivumishi. Data hizo zinawasilishwa kwa muhtasari katika Jedwali Na. 7.

Jedwali Na. 7: Sinonimu za Kategoria ya Kivumishi

Namba	Asili ya Neno		Fahiwa Jumuishi (Kijenzi/vijenzi maana Jumuishi)
	Kiswahili	Kiarabu	
1.	Geni	Ajinabi	A geni Isiyojulikana kabisa
2.	Kavu	Yabisi	Enye kukauka enye ugumu

Chanzo: Data za Maktabani (2020)

Jedwali Na. 7 linaonesha seti 2 za sinonimu zinazohusisha kategoria ya kivumishi. Data hiyo inahusisha maneno ya asili ya Kiswahili na yale ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Kulingana na data hiyo ni dhahiri kuwa kuna ukopaji mdogo wa maneno unaohusisha kategoria ya kivumishi katika lugha ya Kiswahili ambapo maneno yanayokopwa ni machache na zaidi yamekopwa kutoka lugha ya Kiarabu. Maneno hayo ni *ajinabi* na *yabisi*. Kwa hiyo, katika lugha ya Kiswahili kutokana na kutohoa maneno kutoka lugha za kigeni hususani Kiarabu kuna sinonimu zinazohusisha kategoria ya kivumishi. Hata hivyo, kategoria hii haina maneno mengi ya mkopo inapolinganishwa na kategoria za kitenzi na nomino. Kipengele kinachofuata kinafafanua sinonimu zinazohusisha kategoria ya kiunganishi.

4.6 Sinonimu za Kategoria ya Kiunganishi

Kiunganishi ni aina ya maneno inayotumika kuunganisha vipashio vya tungo ili kuunda tungo kubwa zaidi (Khamis, 2009; Kihore, 2009). Katika lugha ya Kiswahili viunganishi vinaweza kuunga vipashio vyenye hadhi sawa au visivyo na hadhi sawa. Vipashio hivyo vyaweza kuwa ni maneno, virai, vishazi au sentensi. Kategoria hii ina sinonimu za asili na za mkopo. Hii inajidhihirisha kupitia data zilizokusanywa ambapo kati ya seti 65 za sinonimu, kuna seti 1 ya sinonimu, sawa na asilimia 2 inayohusisha kategoria ya kiunganishi. Jedwali Na. 8 linawasilisha data hiyo.

Jedwali Na. 8 : Sinonimu za Kategoria ya Kiunganishi

Namba	Asili ya Neno		Fahiwa Jumuishi (Kijenzi/vijenzi maana Jumuishi)
	Kiswahili	Kiarabu	
1.	Pia/vilevile	Aidha	Neno linalounganisha vipashio

Chanzo: Data ya Maktabani na Uwandani (2020)

Jedwali Na. 8 linaonesha seti ya sinonimu inayohusisha kategoria ya kiunganishi. Maneno ya seti hiyo yanajengwa na neno la asili na la mkopo kutoka Kiarabu. Seti hii inajitokeza kwa uchache zaidi katika lugha ya Kiswahili kuliko kategoria zote zilizobainika. Uchache huo unaashiria kuwa kuna utohoaji mdogo wa maneno yanayohusisha kategoria ya kiunganishi kutoka lugha mbalimbali za kigeni ambapo kuna neno moja tu, na hivyo, kuunda seti moja ya sinonimu ya Kiswahili na Kiarabu.

Kwa ujumla, kulingana na data zilizokusanywa na kuchambuliwa imebainika kuwa kuna kategoria za maneno sita zenye sinonimu za asili na za mkopo. Kategoria hizo ni nomino, kitenzi, kielezi, kihisishi, kivumishi na kiunganishi. Kati ya kategoria hizo, imebainika kuwa kategoria ya nomino ndiyo yenye sinonimu nyingi zaidi kuliko kategoria zingine. Sababu mojawapo ya kategoria hii kuwa na seti nyingi za sinonimu ni kuwa kategoria hii inaongoza kwa kukopwa zaidi kuliko kategoria zingine kama kitenzi, kielezi, kiunganishi, kivumishi au kihisishi, na hivyo, kuibua seti nyingi za sinonimu zinazohusisha kategoria ya nomino. Kategoria hii imekopwa karibu kila lugha iliyochangia maneno katika Kiswahili. Haya pia yaliwahi kueleza na McMahan (1994) kuwa maneno mengi yanayokopwa ni ya kategoria ya nomino kuliko kategoria zingine. Hivyo, jambo hili husababisha ongezeko la visawe vya mkopo vinavyohusisha kategoria ya nomino, na hivyo, kuibua seti mbalimbali za sinonimu zenye asili tofauti kwa sababu visawe vingi vya mkopo ambavyo ni vya kategoria ya nomino vinaongezewa juu ya nomino zilizopo katika lugha pokezi.

Khamisi na Kiango (2002) nao waliwahi kueleza kuwa kategoria ya nomino iko wazi na inaongezeka kadiri ya vitu na hali mpya zinavyoingia katika jamii ya Kiswahili na kupatiwa majina au vitambulisho. Kwa hiyo, milango ya kategoria ya nomino iko wazi kupokea nomino mpya kadiri zinavyojitokeza. Jambo hili hapana shaka ndilo linalosababisha ongezeko la visawe kuliko kategoria zingine.

Kategoria inayofuata baada ya nomino, ambayo nayo ina sinonimu nyingi, ni kitenzi. Kategoria hii nayo ina maneno mengi ya mkopo hasa kutoka lugha za kigeni ingawa si sawa na kategoria ya nomino. Kategoria inayofuata baada ya kitenzi ni kielezi ambayo nayo ina seti chache zinazohusisha kategoria hii kisha inafuatia kihisishi, kivumishi na mwisho ni kiunganishi. Kategoria ya kiunganishi ndiyo kategoria yenye maneno machache ya mkopo, na hivyo, kuwa na sinonimu chache zaidi zinazohusisha kategoria hii.

Kategoria sita zilizobainika katika utafiti huu ni zaidi ya zile zilizobainishwa na wataalamu kama McMahan (1994), Kreidler (1998), Gelderen (2002) na Khamisi (2014) ambao hawakubainisha kategoria ya kiunganishi kama ina sinonimu. Hata hivyo, kama walivyoeleza watafiti tangulizi (taz. McMahan, 1994; Kreidler, 1998 na Khamisi, 2014) kuwa kati ya kategoria mbalimbali, nomino ndiyo kategoria yenye sinonimu nyingi zaidi, jambo hilo linajidhihirisha pia katika makala haya

ambapo kategoria hiyo ina sinonimu nyingi kuliko kategoria zingine. Kategoria ya kihisishi ambayo imetajwa na baadhi ya wataalamu kama Gelderen (2002) na Griffith (2006) haijitokezi katika utafiti huu. Kwa hiyo, huenda hakuna sinonimu zinazohusisha kategoria hii katika Kiswahili.

5.0 Hitimisho

Makala haya yamefafanua kategoria za maneno zenye sinonimu za asili na za mkopo katika Kiswahili. Katika uchunguzi huo makala haya yamebaini kuwa kuna kategoria sita za maneno zenye sinonimu za asili na za mkopo. Kategoria hizo ni pamoja na nomino, kitenzi, kielezi, kihisishi, kivumishi na kiunganishi. Kati ya kategoria hizo, matokeo yanaonesha kuwa kategoria ya nomino ndiyo yenye sinonimu nyingi zaidi kuliko kategoria zingine. Mwisho, data za makala haya zimebainisha kuwa kategoria za kiwakilishi na kihusishi hazina sinonimu za asili tofauti katika lugha ya Kiswahili.

Marejeleo

- BAKITA (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Besha, R. M. (1995). "Uingizaji wa Maneno ya Kigeni katika Kiswahili", katika *Kioo cha Lugha*, Juz. 1, 9-14.
- Chacha, L. M. na Malangwa, P. S. (2019). *Semantiki*. Nairobi, Kampala, Dar es Salaam na Kigali: Longhorn Publishers Ltd.
- Chuwa, A. R. (1988). "Foreign Loan Words in Kiswahili", katika *Kiswahili*, Juz. 55/1 na 55/2, 163-172.
- Cruce, A. (2000). *Meaning in Language: An Introduction to Semantics and Pragmatics*. New York: Oxford University Press
- Cruse, A. (2006). *A Glossary of Semantics and Pragmatics*. Edinburgh: Edinburgh University Press.
- Dixon, R. M. W. (1991). *A Semantic Approach to English Grammar*. New York: Oxford University Press.
- Geeraerts, D. (2009). *Theories of Lexical Semantics*. New York: Oxford University Press.
- Gelderen, E. V. (2002). *An Introduction to the Grammar of English: Syntactic Arguments and Socio-Historical Background*. Amsterdam/Philadelphia: John Benjamins Publishing Company.
- Grey, L. H. (1964). *Foundations of Language*. New York: The Macmillan Company.
- Griffiths, P. (2006). *An Introduction to English and Pragmatics*. Edinburgh: Edinburgh University Press.
- Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Harris, R. (1973). *Synonym and Linguistic Analysis*. Toronto na Buffalo: University of Toronto Press.
- Hurford, J. R., Heasley, B., na Smith, M. B. (2007). *Semantics: A Course Book*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Kahigi, K. K. (2019). *Misingi ya Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

- Khamisi, A. M. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi 1*. Dar es Salaam: TUKI.
- Khamisi, A. M. (2014). Chimbuko na Matumizi ya Sinonimu katika Kiswahili Sanifu. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kiango, J. G. (1999). Matatizo ya Utohozi wa Maneno kama Mbinu ya Kukopa Istilahi katika Lugha katika *Mulika*. Juzuu Na. 25, kur. 1-8.
- Kiango, J. G. (1995). Uundaji wa Msamiati Mpya katika Kiswahili: Zoezi lenye Njia Mbalimbali, katika *Kioo cha Lugha*. Juzuu Na. 1, kur. 46-54.
- Kihore, Y. M. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Sarufi 2*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kombo, D. K. na Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Afrika.
- King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kreidler, C. W. (1998). *Introducing English Semantics*. London: Routledge.
- Lyons, J. (1977). *Semantics. Vol. 1*. Cambridge (New York, New Rochelle, Melbourne & Sydney): Cambridge University Press.
- Lyons, J. (1995). *Linguistic Semantics: An Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Massamba, D. P. B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Matei, A.K. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: PPL.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) LTD.
- McMahon, A. M. S. (1994). *Understanding Language Change*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Mohamed, M. A. na Mohamed, S. A. (2014). *Kamusi ya Visawe*. Royapettah: Rathna Offset Printers.
- Ndimele, O. (1997). *Semantics and The Frontiers of Communication*. Port Harcourt: University of Port Harcourt Press Ltd.
- Palmer, F. R. (1976). *Semantics*. 2nd Edition. Cambridge: Cambridge University Press.
- Ragin, C. C. (1987). *The Comparative Method*. California: University of California Press.
- Resani, M. (2015). *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Print Technology.
- Riemer, N. (2010). *Introducing Semantics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Robins, R. H. (1980). *General Linguistics*. London: Longmans.
- Saeed, J. I. (1997). *Semantics, Toleo la 2*. Blackwell: Blackwell PUBLISHING Limited.
- Sarma, S. K., Bharali, H., Mahanta, M., Sikia, U., na Sarmah, D. (h.t). "An Analytical Study of Synonymy in Assamese Language Using WorldNet: Classification and Structure". Makala imesomwa mtandanoni katika <https://aclanthology.org/W14-0134.pdf>

- Skallman, E. (2012). The Interplay of Synonymy and Polysemy: The Case of Arrojar, Echar, Ianzar and Tirar. *Tasinifu ya Umahiri* (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Tromso.
- TUKI (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi: OUP.
- Ullmann, S. (1967). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. London: Oxford.